| Neno | Maana | Picha |
|---|---|---|
| **Breli** | Mfumo wa kusoma unaotumiwa na mtu asiyeona. Herufi zimeandikwa kwa nuktatundu. Mtu anaweza kupapasa hizi doti kwa kutumia sehemu ya juu ya vidole. | |
| **Miwani ya kusomea iliyoshauriwa na daktari** | Miwani ambayo ni mahususi kwa mtu anayeivaa baada ya mtaalam kufanya uchunguzi wa kina kwa mhusika. |  |
| **Tatizo la kuona mbali/na karibu** | Ni tatizo la Uoni linalotokea mara kwa mara kwa watu. Tatizo hili linaweza kurekebishwa kwa kutumia miwani sahihi au lenzi zinazovaliwa moja kwa moja kwenye macho. Kuna aina tofauti za matatizo ya kuona karibu na mbali na karibu ikiwemo astigmatism, hyperopia, myopia and presbyopia. | |
| **Astigmatism** | Watu wenye astigmatism wanapata ugumu kuona vizuri kwa kuona mbali na karibu. |  |
| **Hyperopia** | Hyperopia inajulikana pia kama uwezo wa kuona mbali. Watu wenye hyperopia wanaweza kuona vizuri vitu vilivyoko mbali. Hatahivyo wanapata taabu kuona vitu ambavyo viko karibu. |  |
| **Myopia** | Myopia inajulikana pia kama uwezo wa kuona karibu. Watu wenye myopia wanaweza kuona vizuri vitu vilivyo karibu. Hatahivyo,wanaona ukungu kwenye kuangalia vitu vilivyo mbali. |  |
| **Presbyopia** | Presbyopia .inatokea kwa watu wengi kwa kadri wanakuwa kiumri. Watu wenye presbyopia wanapata taabu kuona vitu vilivyo karibu. Kwa mfano, shughuli kama vile kusoma na kushona zinafanyika kwa taabu. | |
| **Uoni** | Uwezo wa kuona. | |
| **Matatizo ya Uoni** | Matatizo mbalimbali ya Uoni ni pamoja na matatizo ya Afya ya Macho, Uoni wa mbali au Uoni wa karibu. Matatizo mengi ya Uoni yanaweza kuepukika kwa kinga, matibabu sahihi na/ au vifaa Saidizi. Baadhi ya matatizo | |

| | | |
|---|---|---|
| | ya Uoni hayawezi kuepukika. Hii inamaanisha kuwa ni vigumu kurudisha Uoni kamili kama ilivyokuwa hapo awali. | |